ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

## *Mapitio ya Nusu Mwaka 2023/24*

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2024**

ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*

*2023/24*

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2024**

## Utangulizi

Tamko la Sera ya Fedha lililotolewa na Benki Kuu mwezi Juni 2023, lilibainisha malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2023/24 kuwa ni kuhakikisha utulivu wa bei na kuchangia ukuaji endelevu wa uchumi. Mfumuko wa bei ulipangwa kufikia kiwango kisichozidi asilimia 5 na ukuaji wa uchumi ulitarajiwa kuwa asilimia 5 mwaka 2023 na asilimia 5.5 mwaka 2024 kwa Tanzania Bara, baada ya mapitio yaliyofanyika mwezi Novemba 2023. Kwa upande wa Zanzibar, ukuaji wa Pato la Taifa ulitarajiwa kuwa asilimia 7.1 na asilimia 7.4 kwa mwaka 2023 na 2024, mtawalia.

Taarifa hii ya Mapitio ya Nusu Mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha la mwaka 2023/24, inaainisha tathmini ya mwenendo wa uchumi wa dunia, utekelezaji wa sera ya fedha na mwenendo wa uchumi hapa nchini. Aidha, taarifa hii inatoa mwelekeo wa mwenendo wa uchumi wa dunia, uchumi wa Tanzania, na sera ya fedha katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2023/24.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Ukuaji wa uchumi wa dunia haukuwa wa kuridhisha katika kipindi cha mwaka 2023. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi ilitofautiana kwa kiwango kikubwa baina ya nchi. Kulingana na taarifa za Benki ya Dunia (WB), Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), na Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), ukuaji wa uchumi ulikuwa asilimia 2.6, asilimia 3.1, na asilimia 2.9 mwaka 2023, mtawalia. Ukuaji huu ni tofauti na ukuaji wa asilimia 3.3, asilimia

3.5 na asilimia 3.3, mwaka uliotangulia. Ukuaji wa uchumi wa nchi za Afrika, kusini mwa jangwa la Sahara, ulikuwa asilimia 3.3 kutoka asilimia 4. Mwenendo huu ulichangiwa na migogoro ya kimataifa na utekelezaji wa sera ya fedha katika nchi zilizoendelea, uliolenga kudhibiti mfumuko wa bei kwa kupunguza ukwasi.

Mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi, kufuatia utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kupunguza ukwasi pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Kulingana na Taarifa ya Hali ya Uchumi ya IMF ya mwezi Januari 2024, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 6.8 mwaka 2023 kutoka asilimia 8.7 mwaka 2022. Katika nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 4.6 kutoka 7.3. Licha ya kupungua, kiwango hicho kilibaki juu ya lengo la asilimia 2. Nchi nyingi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ziliweza kufikia malengo ya mfumuko wa bei ya kikanda.

Bei za bidhaa katika soko la dunia ziliendelea kupungua katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24. Mathalan, bei ya mafuta ghafi ya nishati ilipungua kufikia wastani wa dola za Marekani 83.7 kwa pipa ikilinganishwa na dola 90.8 kwa pipa katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Hali hii ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa hiyo katika baadhi ya nchi waagizaji wakubwa duniani kama China, licha ya makubaliano ya nchi za OPEC+ ya kupunguza uzalishaji. Bei ya dhahabu iliendelea kuwa juu kufikia wastani wa dola za Marekani 1,952.4 kwa wakia, ukilinganisha na dola 1,727.3 kwa wakia kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Hali hii ilitokana na kushuka kwa thamani ya dola ya Marekani kufuatia benki kuu

ya nchi hiyo kulegeza utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kupunguza ukwasi kwenye uchumi.

**Utekelezaji wa Sera ya Fedha Katika Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2023/24**

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, Benki Kuu ya Tanzania ilitekeleza sera ya fedha ya kupunguza ongezeko la ukuaji wa ukwasi katika uchumi, kama ilivyoainishwa katika Tamko la Sera ya Fedha lililochapishwa mwezi Juni 2023. Lengo la utekelezaji wa sera hii lilikuwa ni kudhibiti mfumuko wa bei kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na kuendelea kuchangia ukuaji wa uchumi. Lengo la mfumuko wa bei lilikuwa asilimia 5 kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Uchumi ulitarajiwa kukua kwa asilimia 5 mwaka 2023 na asilimia 5.5 kwa mwaka 2024 kwa Tanzania Bara. Kwa Zanzibar, ukuaji wa uchumi ulitarajiwa kuwa asilimia 7.1 na 7.4, mtawalia. Kutokana na malengo haya, utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga:

i. ukuaji wa fedha taslimu wa asilimia 10.1;
ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.1; na
iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 16.4.

Aidha, Benki Kuu ililenga kuendelea kuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni kuweza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Utekelezaji wa sera ya fedha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24 uliweza kufikia malengo yaliyokusudiwa, licha ya kukabiliwa na changamoto zilizotokana na mwenendo usioridhisha wa uchumi wa dunia. Ukwasi katika uchumi ulitosheleza mahitaji ya shughuli za uzalishaji na kuwezesha benki za biashara kutoa mikopo kwa sekta binafsi. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 15.5 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, ukilinganishwa na lengo la asilimia 10.1 kutokana na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kuliko ilivyotarajiwa. Kwa mwaka 2023, ukuaji wa M3 ulikuwa asilimia 14.1 ukilinganisha na asilimia 11.6 kwa mwaka 2022.

Mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka, kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 19.2 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24. Ukuaji huo ulikuwa zaidi ya makadirio ya ukuaji wa asilimia 16.4. Katika mwaka 2023, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 17.1 ukilinganisha na asilimia 22.5 mwaka 2022. Uwiano wa mikopo kwa Pato la Taifa ulifikia takriban asilimia 18.8 ukilinganishwa na asilimia 16.1 mwaka 2022. Ukuaji huu ulitokana na maboresho katika mazingira ya biashara na kuimarika kwa shughuli za uchumi nchini. Riba katika soko la fedha baina ya mabenki na masoko ya mitaji ziliongezeka, wakati viwango vya riba za mikopo inayotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi havikuwa na mabadiliko makubwa. Vilevile, utekelezaji wa sera ya fedha uliwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa katika programu ya *Extended Credit Facility (ECF*) ya IMF inayotekelezwa na Serikali.

Kwa upande wa akiba ya fedha za kigeni, Benki Kuu pia ilifanikiwa kufikia lengo, ambapo akiba ilikuwa ya kutosha katika kipindi chote cha nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24. Akiba hiyo ilifikia dola za Marekani bilioni 5.5 mwezi Desemba 2023 ikilinganishwa na dola bilioni 5.4 mwezi Juni 2023. Kiwango hiki kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa miezi 4.5, ikiwa ndani ya lengo la nchi na lile la Jumuiya ya Afrika Mashariki la angalau miezi 4 na miezi 4.5, mtawalia.

Thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilikuwa imara, japokuwa ilipungua kama ilivyokuwa katika nchi nyingi zinazoendelea. Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2023, thamani ya shilingi ilipungua kwa kasi kutokana na ongezeko kubwa la mahitaji ya dola za Marekani yaliyotokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta ghafi ya nishati katika soko la dunia. Aidha, fedha hiyo ilipungua katika soko la fedha za kigeni nchini kutokana na uamuzi wa benki kuu ya Marekani kuendelea kutekeleza sera ya kupunguza ukwasi katika kukabiliana na mfumuko wa bei. Changamoto hii ilipungua katika miezi mitatu ya mwisho ya mwaka 2023 kutokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii, mauzo ya bidhaa, pamoja na Serikali kupata mikopo na misaada kutoka nje ya nchi. Vilevile, Benki Kuu ilichukua hatua mbalimbali zilizowezesha kuongeza fedha za kigeni katika soko. Kwa ujumla, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya ilipungua kwa asilimia 6.4 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24 na asilimia 8.2 kwa mwaka 2023.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

### Tanzania Bara

Mwenendo wa uchumi wa Tanzania Bara uliendelea kuwa wa kuridhisha, licha ya changamoto zinazotokana na mwenendo wa uchumi wa dunia usioridhisha. Katika robo tatu za kwanza za mwaka 2023, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 5.3. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, huduma za kifedha na bima, na uchimbaji wa madini. Kutokana na mwenendo huu na viashiria vya uchumi katika robo ya nne ya mwaka 2023, lengo la ukuaji wa uchumi la asilimia 5 katika mwaka 2023 litakuwa limefikiwa.

Mfumuko wa bei uliendelea kubakia ndani ya lengo la nchi na malengo ya nchi za EAC na SADC. Mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.2 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2023, ukilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Katika mwaka 2023, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3 ukilinganisha na asilimia 4.9 kwa mwaka uliopita. Hali hii ilitokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na ya kibajeti, uwepo wa chakula cha kutosha nchini, na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.

Utekelezaji wa bajeti ya Serikali ulikuwa wa kuridhisha. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya 2023/24, mapato ya ndani yanayojumuisha mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, yalikuwa shilingi bilioni 14,754.9, sawa na asilimia 95.8 ya lengo. Mapato ya kodi yalikuwa asilimia

98.6 ya lengo. Mwenendo wa kuridhisha wa mapato ulitokana na hatua zilizochukuliwa kuimarisha usimamizi wa kodi na kuimarika kwa shughuli za uchumi. Serikali iliendelea kupanga matumizi kulingana na mapato. Kutokana na utaratibu huu, matumizi ya Serikali yalikuwa asilimia 95.2 ya makadirio. Matumizi kwa shughuli za maendeleo yalikuwa ni asilimia 43.8 ya matumizi yote ya Serikali. Nakisi ya bajeti iligharamiwa na mikopo kutoka ndani na nje ya nchi.

Deni la Serikali limeendelea kuwa himilivu kwa mujibu wa vigezo vyote vya upimaji vinavyokubaliwa kimataifa. Deni la Serikali lilipungua kufikia dola za Marekani milioni 34,791.9 mwezi Desemba 2023 kutoka dola za Marekani milioni 35,222.6 mwezi Juni 2023. Deni la nje lilikuwa asilimia 64.8. Deni la nje la seka binafsi lilikuwa dola za Marekani milioni 6,957.6 kutoka dola za Marekani milioni 7,425.2. Sehemu kubwa ya mikopo hii ilielekezwa katika utekelezaji wa miradi ya usafirishaji na mawasiliano, huduma za jamii, na nishati na madini. Deni la ndani la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 30,676.3 ukilinganisha na shilingi bilioni 28,927.1 mwezi Juni 2023, ambapo takriban asilimia 85 ya deni ilikuwa ni dhamana za Serikali.

Sekta ya nje iliimarika, licha ya changamoto zilizotokana na kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan mafuta ghafi ya nishati, pamoja na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika nchi zilizoendelea ili kukabiliana na mfumuko wa bei. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida *(current account)* ilikuwa dola za Marekani milioni 1,096, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni

3,085 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi, ongezeko la mapato ya shughuli za utalii na mauzo ya bidhaa nje ya nchi hususan dhahabu, kahawa na tumbaku. Nakisi ya urari wa malipo inatarajiwa kuendelelea kupungua. Hali hii inatokana na matarajio ya kuendelea kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan nishati na chakula. Aidha, mauzo ya bidhaa nje ya nchi yanatarajiwa kuongezeka kufuatia utekelezaji wa mikakati ya kuongeza uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi. Katika kipindi cha muda wa kati, nakisi hii inatarajiwa kuwa wastani wa asilimia 3.2 ya Pato la Taifa.

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalikuwa dola za Marekani milioni 7,840.7 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24 ukilinganisha na dola milioni 6,643 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko hili lilitokana na mapato yatokanayo na shughuli za utalii, mauzo ya korosho, tumbaku, kahawa na dhahabu. Katika mwaka 2023, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalikuwa dola za Marekani milioni 13,976 ukilinganisha na dola milioni 11,985.8 kwa mwaka uliotangulia. Kiwango hiki kilikuwa ni sawa na asilimia 17 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 16 mwaka 2022. Bidhaa nyingi ziliuzwa India, Afrika Kusini, Falme za Kiarabu, Uswisi na China.

Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi zilikuwa dola za Marekani milioni 8,484.1 katika nusu mwaka wa 2023/24, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,405.8

katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia. Kupungua huku kulichangiwa na kushuka kwa bei ya bidhaa katika soko la dunia, hususan, bidhaa za mafuta ghafi ya nishati, mbolea, na huduma za usafirishaji. Katika mwaka 2023, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa nje ya nchi zilikuwa dola za Marekani milioni 16,058.7 ukilinganisha na dola milioni 16,674.1 kwa mwaka uliotangulia. Kiwango hiki kilikuwa ni sawa na asilimia 19.2 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 22.6 mwaka 2022. Bidhaa nyingi ziliagizwa kutoka China, India, Falme za Kiarabu, Saudia na Japani.

Sekta ya fedha imeendelea kuwa imara huku viashiria hatarishi vikipungua kutokana na matarajio ya kuendelea kuimarika kwa uchumi. Sekta ya kibenki ambayo ni sehemu kubwa ya sekta ya fedha imeendelea kuwa imara, yenye kutengeneza faida, ukwasi na mtaji wa kutosha. Amana, mikopo na rasilimali pia ziliendelea kuongezeka. Vilevile, ubora wa rasilimali uliendelea kuongezeka, ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulipungua hadi asilimia 4.3 mwezi Desemba 2023 kutoka asilimia 5.5 mwezi Juni 2023. Hali hii inaashiria kuendelea kupungua kwa vihatarishi katika utoaji wa mikopo kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi pamoja na hatua za kisera na kiusimamizi zinazochukuliwa na Benki Kuu katika kupunguza mikopo chechefu. Kiwango cha mikopo chechefu kinategemewa kuendelea kupungua kutokana na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathirika na mtikisiko wa kiuchumi duniani na hatua zinazochukuliwa na benki na taasisi za fedha katika kukabiliana na changamoto hii.

Mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi na Benki Kuu iliendelea kuifanyia maboresho. Maboresho haya yanaendelea kufanyika ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu, kurahisisha ufuatiliaji na usimamizi, na kuendelea kuongeza idadi ya wananchi wanaofikiwa na huduma rasmi za kifedha. Wakati huohuo, Benki Kuu imeendelea na utekelezaji wa mradi wa Mfumo wa Malipo ya Papo Hapo *(Tanzania Instant Payment System)*, ambao unaendelea kurahisisha malipo madogomadogo kwa usalama na ufanisi baina ya watoa huduma za fedha kwa njia ya kidigitali. Hadi Desemba 2023, mfumo huu umeshajumuisha watoa huduma za kifedha 45 kutoka 40 kwa mwaka 2022. Aidha, simu za mkononi zimeendelea kuwa kichocheo kikubwa katika kuongeza huduma jumuishi za fedha nchini na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha.

**Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar**

Katika robo tatu za kwanza za mwaka 2023, uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za huduma za malazi na chakula, ujenzi, na uzalishaji viwandani. Uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kuendelea kuimarika katika robo ya nne ya mwaka 2023, kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuimarika kwa shughuli za utalii na uzalishaji viwandani.

Mfumuko wa bei ulipungua na kukaribia kufikia lengo la asilimia 5. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 6.5 ukilinganisha na asilimia 6.7 kwa kipindi kama

hicho mwaka uliotangulia. Katika mwaka 2023, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 5.5 ukilinganisha na asilimia 8.1 katika mwaka uliotangulia. Mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za chakula. Vilevile, mfumuko wa bei za chakula ulipungua, japo ulibaki kuwa juu kutokana na madhara ya kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na kushuka kwa thamani ya shilingi.

Utekelezaji wa bajeti ya Serikali umeendelea kuwa wa kuridhisha. Mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 709.8, sawa na asilimia 99.1 ya lengo. Mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 628.3, sawa na asilimia 101.1 ya lengo. Aidha, mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 81.5, sawa na asillimia 86.2 ya lengo. Mafanikio haya yamechangiwa na kuimarika kwa usimamizi wa kodi na ongezeko la matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji mapato. Misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo ilikuwa ni shilingi bilioni 26.8. Serikali iliendelea kufanya matumizi kulingana na mapato. Matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 1,079, ambapo asilimia 47.1 ya matumizi yote zilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Nakisi ya bajeti iligharamiwa na mikopo ya ndani na nje ya nchi. Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 3,382.1 mwezi Desemba 2023, kutoka shilingi bilioni 2,737.9 mwezi Juni 2023, ambapo deni la nje lilikuwa ni asilimia 76.2.

Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilikuwa dola za Marekani milioni 207.9 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2023, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 177.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa na kushuka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Hata hivyo, mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka kwa asilimia 5.9 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya 2023/24 yakiakisi ongezeko la shughuli za utalii.

## Matarajio ya Hali ya Uchumi wa Dunia

Ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kutokuwa wa kuridhisha kwa mwaka 2024, na utatofautiana kwa kiwango kikubwa baina ya nchi. Kulingana na taarifa za WB, IMF, OECD uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 2.4, asilimia 3.1, na asilimia 2.7 katika mwaka 2024, mtawalia. Ukuaji wa uchumi katika nchi za Afrika, kusini mwa jangwa la Sahara, unatarajiwa kufikia asilimia 3.8. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi katika baadhi ya nchi inatokana na migogoro ya kimataifa na utekelezaji wa sera ya fedha yenye lengo la kupunguza ukwasi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua. Katika nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei unaweza kuzidi lengo la asilimia 2, licha ya kuendelea kupungua. Kwa muktadha huu, benki kuu katika nchi hizo zinatarajiwa kuendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kupunguza ukwasi kwa kasi ndogo kuliko kipindi kilichopita au kutoendelea kuongeza riba ya sera ya fedha. Nchi nyingi za EAC na SADC zinatarajiwa kuwa na mfumuko wa bei unaoendana na malengo ya kikanda. Bei ya mafuta

ghafi ya nishati inatarajiwa kuendelea kupungua kufikia takriban dola za Marekani 80 kwa pipa katika mwaka 2024. Matarajio haya yatategemea uamuzi wa nchi wanachama wa OPEC+ na mahitaji. Bei ya dhahabu inatarajiwa kuendelea kuwa juu, kufikia wastani wa dola za Marekani 1,900 kwa wakia.

**Matarajio ya Hali ya Uchumi wa Tanzania**

Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kuimarika. Ukuaji wa uchumi wa Tanzania Bara unatarajiwa kuwa asilimia 5.5 mwaka 2024, na asilimia 7.4 kwa Zanzibar. Matarajio haya yanatokana na uwekezaji unaoendelea katika sekta binafsi na ya umma, hatua mbalimbali za kuboresha mazingira ya kibiashara, uwepo wa mvua za kutosha katika maeneo mengi nchini na kuendelea kuimarika kwa shughuli za utalii. Aidha, kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwemo mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Julius Nyerere kutachangia kuendelea kuimarika kwa uchumi. Hata hivyo, matarajio ya ukuaji wa uchumi yanaweza kuathiriwa na migogoro ya kimataifa na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kupunguza ukwasi katika nchi zilizoendelea.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa wa kiwango cha chini, sawia na lengo la asilimia 5 katika mwaka 2024. Hali hii inatokana na uwepo wa chakula cha kutosha nchini, kutengemaa kwa bei za bidhaa katika soko la dunia hususan mafuta ghafi na chakula, utekelezaji wa sera ya fedha, na utulivu wa viwango vya kubadilisha fedha. Maoteo haya yanaweza kuathiriwa na mwenendo wa bei za

mafuta ghafi ya nishati katika soko la dunia kutokana na maamuzi ya nchi za OPEC+ na mahitaji. Aidha, migogoro ya kimataifa inayoendelea inaweza kuchangia mabadiliko katika maoteo haya.

Akiba ya fedha za kigeni inatarajiwa kuendelea kuwa imara na kuendana na malengo ya nchi. Hali hii inatokana na matarajio ya kuendelea kutengemaa kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na utekelezaji wa mikakati ya kuongeza mauzo nchi za nje *(export promotion)* na kupunguza uagizaji wa bidhaa ambazo zinazalishwa nchini *(import substitution)*.

**Utekelezaji wa Sera ya Fedha katika Nusu ya Pili ya Mwaka 2023/24**

Kutokana na mwenendo wa uchumi wa dunia na hapa nchini, utekelezaji wa sera ya fedha katika nusu ya pili ya mwaka 2023/24 unatarajiwa kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei kuwa ndani ya lengo la asilimia 5. Aidha, sera ya fedha itaendelea kuchangia ukuaji wa uchumi kufikia lengo la asilimia 5.5 mwaka 2024. Kufuatia kuanza utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa kutumia riba (*interest rate-based monetary policy framework*), Kamati ya Sera ya Fedha *(MPC)* ya Bodi ya Benki Kuu ya Tanzania ilipanga Riba ya Benki Kuu (*Central Bank Rate)* kuwa asilimia 5.5 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024. Riba hii imezingatia malengo ya mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi. Riba ya Benki Kuu kwa robo ya pili ya mwaka 2024 itatangazwa mwezi Aprili 2024. Benki Kuu itahakikisha utulivu katika kiwango cha riba za mikopo ya siku 7 katika soko la

fedha baina ya mabenki (*interbank market*). Benki Kuu itaendelea kuhakiksha kuwa utekelezaji wa sera ya fedha unaendana na malengo ya programu ya *Extended Credit Facility (ECF)* ya IMF inayotekelezwa na Serikali.

## Riba na Thamani ya Shilingi Dhidi ya Fedha za Kigeni

Riba zinazotozwa na taasisi za fedha nchini zitaendelea kuamuliwa kwa nguvu ya soko. Hivyo, utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia mfumo wa riba hauna lengo la kuweka ukomo katika viwango vya riba. Badala yake, mfumo huo utachangia katika kuwezesha taasisi za fedha kupanga riba kwa kuzingatia nguvu ya soko. Thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni pia itaendelea kuamuliwa na nguvu ya soko. Benki Kuu itashiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni baina ya mabenki *(interbank foreign exchange market)* kama nyenzo ya kutekeleza sera ya fedha au kuimarisha akiba ya fedha za kigeni.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Benki Kuu ya Tanzania, 16 Barabara ya Jakaya Kikwete 40184,
S. L. P 2302, Dodoma, Tanzania
Barua pepe: botcommunications@bot.go.tz
Tovuti: https://www.bot.go.tz